KY Standards

Your home for Kentucky Academic Standards.

KYstandards.org

standards@education.ky.gov

facebook.com/kydeptofed

@KyDeptofEd

# Karibu kwenye Shule ya Sekondari

## Mwongozo wa Familia kwa Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky

Mwongozo huu uliundwa ili kusaidia familia kuelewa *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* na kuonyesha kile ambacho watoto watajifunza kufikia mwisho wa shule ya sekondari. Ala hii inatoa taarifa kuhusu mawazo na mastadi muhimu ambazo walimu wataanzisha katika hesabu, kusoma na kuandika, sayansi na masomo ya kijamii. Inajumuisha mifano inayowezekana ya kile wanafunzi wataombwa kufanya darasani, jinsi ya kumsaidia mtoto wako nyumbani, maswali unayoweza kumuuliza mwanafunzi wako wa shule ya sekondari na maswali ambayo familia zinaweza kumuuliza mwalimu wa mtoto wao.

Mwongozo huu pia uliundwa ili kuwasaidia wazazi kuelewa jinsi wanavyoweza kufanya kazi na walimu kusaidia majifunzo ya mwanafunzi wao wa shule ya sekondari. Walimu na familia wanapofanya kazi pamoja ili kuwasaidia wanafunzi kufahamu *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky*, wanafunzi wanaweza kufaulu kwa kukuza ujuzi watakaohitaji maishani baada ya kuhitimu.

Ikiwa una maswali kuhusu maelezo haya au ikiwa mtoto wako anahitaji usaidizi wa ziada, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako.

### Kwa nini Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky ni Muhimu?

*Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* ni muhimu kwa sababu vinasaidia kuhakikisha kwamba wanafunzi wote, haiduru wanaishi wapi au wanasoma shule gani, wana ujuzi wanaohitaji ili kupata maisha bora ya baadaye. Viwango vinawakilisha lengo au matokeo ya eneo la somo (kama vile hesabu, kusoma na kuandika, sayansi na masomo ya kijamii). Zinasaidia kuweka matarajio ya wazi na thabiti kwa kile ambacho wanafunzi wanapaswa kujua na kuweza kufanya kuanzia shule ya chekechea hadi shule ya sekondari. Viwango si mtaala na havibainishi muundo wa mpango wa somo au jinsi vitengo vinapaswa kupangwa. Maamuzi ya jinsi bora ya kuwasaidia wanafunzi kufikia malengo katika viwango yanaachiwa wilaya ya shule za mitaa na walimu.

### Viwango vimepangwa vipi?

*Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* vimepangwa tofauti kulingana na eneo la maudhui. Baadhi ya *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* yamepangwa darasa kwa darasa, pale nyingine zikiwekwa katika viwango kadhaa vya darasa, kama vile "shule ya sekondari" kwa darasa 9-12. Katika masomo yote, viwango vinaonyesha kile ambacho wanafunzi wanapaswa kujifunza na kuweza kufanya, lakini si jinsi uzoefu huo wa kujifunza unapaswa kutengenezwa au ni nyenzo gani zinafaa kutumia. Kwa maelezo zaidi kuhusu *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* tembelea https://kystandards.org/ ili kusoma viwango kamili na kupata nyenzo zinazohusiana na viwango.

# Hesabu ya Shule ya Sekondari

## Muhtasari wa Aljebra 1:

Wakati wa Aljebra 1, wanafunzi wataendelea kujenga na kupanua dhana zinazoendelezwa katika shule ya kati [middle school]. Mtoto wako ata:

- Andika na kutatua milinganyo ya kuunda grafu kadri zinavyoonyesha hali halisi ya ulimwengu;
- Chunguza utendakazi wa “quadric” na kielelezo; na
- Zingatia kiwango fulani cha usahihi, iwe hiyo inaonyeshwa kwa kutumia vitengo ipasavyo au kuchagua kiwango cha kuridhisha wakati wa kuunda grafu.

Kumbuka: Ikiwa mtoto wako anasoma shule inayotoa njia iliyojumuishwa mlolongo wa kitamaduni zaidi, mtoto wako anapaswa kuwa anajifunza viwango vyovyote vilivyowekwa lebo ya Aljebra 1 au Jiometri kufikia mwisho wa Hesabu 2 iliyojumuishwa.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni:

• Kutumia mbinu mbalimbali kutatua mifumo ya milinganyo na kukosekana kwa usawa;
• Kutumia viwakilishi vingi (milinganyo, majedwali, grafu) kuwakilisha utendakazi (shughuli);
• Kutatua, kuchora grafu na kulinganisha milinganyo ya mstari, ya kielelezo na ya “quadratic” na utendakazi; na
• Kutumia milinganyo ya mstari, ya “quadratic” na ya kielelezo kwa hali za ulimwengu halisi ili kutatua matatizo, kuunda dhana na kujibu maswali.

## Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani:

• Hesabu inaweza kuwa changamoto. Mhimize mtoto wako kutokata tamaa hadi mikakati na zana nyingi ziwe zimekamilika.
• Kumbuka, uzoefu wako na hesabu - iwe chanya au hasi - haufafanui uzoefu wa mtoto wako.
• Njia mojawapo ya kufanikiwa katika hesabu ni kutorudi nyuma. Mhimize mtoto wako kuwa makini, kuuliza maswali na kuendelea kufikia aliye mbele wakati wa darasa.
• Tafuta usaidizi nje ya darasa kutoka kwa mwalimu kabla au baada ya shule na kutoka kwa nyenzo za mtandao.

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

• Je, ni baadhi ya mambo gani ambayo yanatofautiana na ni mambo gani ambayo yanabaki sawa?
• Iwapo ulilipwa senti siku ya kwanza, senti mbili siku ya 2, senti nne siku ya 3 na kila siku malipo yako yaliendelea kuongezeka mara mbili, hadi lini upate $100?
• Je, ulijaribu mbinu ngapi kuhusu tatizo hili?
• Je, jibu hili linaonekana kuwa sawa kwa hali hiyo?

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mwalimu wa Mtoto Wako:

• Je, mtoto wangu ameacha kwa urahisi kazi ngumu?
• Mtoto wangu anapaswa kutumia muda gani kufanya kazi za nyumbani kila usiku?
• Unafikiri ni nini kinachompa mtoto wangu shida zaidi? Je, ninaweza kumsaidiaje kufanya maendeleo katika eneo hili?
• Je, kuna zana zozote (nyenzo, tovuti, video, n.k.) tunazoweza kutumia nyumbani kumsaidia?
• Je, tunawezaje kufikia Desmos? (Desmos ni kikokotoo cha mtandaoni ambacho wanafunzi wataweza kufikia wakati wa tathmini zijazo)? Je, kuna vipengele vyovyote ambavyo tunapaswa kutumia nyumbani kusaidia ujifunzaji darasani?
• Mtoto wangu atakuwa anajifunza nini mwaka huu? Ninawezaje kusaidia ukuaji wa mtoto wangu katika eneo hilo?

## Muhtasari wa Jiometri:

Wakati wa Jiometri, wanafunzi watajenga juu ya dhana kutoka kwa jiometri ya shule ya kati wanapoendea kufanya kazi kwa pembe, mistari na aina mbalimbali ya maumbo ya pande mbili na tatu (dimensional):

# Hesabu ya Shule ya Sekondari

- Chunguza nadharia zinazohusiana na ulinganifu na ufanano kwa undani zaidi kupitia mabadiliko na ujenzi;
- Anzishwa kwa uwiano msingi wa Trigonometri kujifunza jinsi uwiano huo unavyoweza kutumiwa kutatua matatizo za ulimwengu halisi; na
- Tumia aina mbalimbali za dhana nyingine za kijiometri ili kuiga na kutatua hali mbalimbali za ulimwengu halisi.

Kumbuka: Iwapo mtoto wako anasoma shule inayotowa njia iliyojumuiishwa mlolongo wa kitamaduni, mtoto wako anapaswa kuwa anajifunza viwango vyovyote vilivyowekwa lebo ya Aljebra 1 au Jiometri kufikia mwisho wa Hesabu 2 iliyojumuishwa.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni:

• Kutumia viwianishi kutafuta mteremko, umbali na sehemu ya kati kati ya pointi mbili na kuhalalisha mistari sambamba na ya mstatili;
• Kuelewa athari za mabadiliko katika randa;
• Kutumia nadharia za mistari, pembe, pembetatu na msambamba;
• Kuunda na kutumia miundo ya kijiometri;
• Kuelezea uhusiano kati ya pembe tofauti na mduara unaolingana;
• Kuelewa uhusiano kati ya uwakilishi wa miduara ya kialjebra na kijiometri; • Kutumia sifa za kufanana ikijumuisha upanuzi; na
• Kuelewa sifa za pembetatu za kulia.
.

## Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani:

• Hesabu inaweza kuwa changamoto. Mhimize mtoto wako kutokata tamaa hadi mikakati na zana nyingi ziwe zimekamilika.
• Kumbuka, uzoefu wako na hesabu (iwe chanya au hasi) haufafanui uzoefu wa mtoto wako.
• Njia mojawapo ya kufanikiwa katika hesabu ni kutorudi nyuma. Mhimize mtoto wako kuwa makini, kuuliza maswali na kuendelea kufikia aliye mbele wakati wa darasa.
• Tafuta usaidizi nje ya darasa kutoka kwa mwalimu kabla au baada ya shule na kutoka kwa nyenzo za mtandao.

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

• Ni nini kinachofanya maumbo mawili kuwiana (sawa sawa)? (Toa mfano wa vitu viwili sawa sawa.)
• Ni nini kinachofanya maumbo mawili kufanana? (Toa mfano wa vitu viwili vinavyofanana.)
• Toa mfano wa ulimwengu halisi wa vitu viwili vilivyosambamba. Je, kuna sababu au faida ya kuwa na vitu hivyo kuwa sambamba?
• Je, unaweza kuanza na mduara wa saizi yoyote na kuunda mduara wa saizi nyingine kwa kubadilisha mizani?

## Maswali Unayoweza Kumuuliza mwalimu wa Mtoto Wako:

• Je, mtoto wangu anajifunza vyema zaidi kwa kuchunguza dhana za kijiometri mwenyewe au kwa teknolojia?
• Je, mtoto wangu ana shida ya kuona dhana za kijiometri?
• Mtoto wangu anapaswa kutumia muda gani kufanya kazi za nyumbani kila usiku?
• Unafikiri ni nini kinachompa mtoto wangu shida zaidi? Je, ninaweza kumsaidiaje kufanya maendeleo katika eneo hili?
• Je, kuna zana zozote (nyenzo, tovuti, video, n.k.) ambazo tunaweza kutumia nyumbani?
• Desmos ni nini? Je, kuna vipengele vyovyote ambavyo tunapaswa kutumia mahususi nyumbani kusaidia ujifunzaji darasani?
• Je, ni viwango gani vya ufasaha ambavyo mtoto wangu atakuwa akijifunza mwaka huu? Je, ninawezaje kusaidia ukuaji wa mtoto wangu wa ufasaha katika eneo hilo?

## Muhtasari wa Baada ya Msingi:

# Hesabu ya Shule ya Sekondari

Aljebra 1 na Jiometri zinachukuliwa kuwa kozi za msingi za hesabu huko Kentucky. Kukamilisha Aljebra 1, Jiometri na kozi mbili za baada ya msingi zinapaswa kukidhi mahitaji yote yaliyobainishwa katika Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky vya Hesabu. Wakati wa kozi za baada ya msingi, wanafunzi watajenga na kupanua dhana zilizotengenezwa katika kozi za msingi. Mtoto wako ata:

- Panua juu ya miundo ya mstari, "quadratic" na kielelezo ili kujihusisha kwa kina zaidi na polynomia za hali ya juu, misemo ya "logarithm" na mantiki, milinganyo na utendakazi; na
- Chunguza takwimu na dhana za uwezekano na jinsi dhana hizo zinavyotumika katika hali halisi za ulimwengu.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni:

• Kuelewa dhana ya namba changamano na kusuluhisha milinganyo ya "quadratic" ambayo ina majibu changamano;
• Kutumia "matrices" kuwakilisha data na kuwa na uwezo wa kufanya shughuli na "matrices";
• Kutumia umbo uliobainishwa wa usemi, wakati wowote inapowezekana, kutafuta mizizi ya milinganyo na/au sufuri kwa vitendakazi;
• Kuwakilisha, kupanga na kutafuta mienendo katika data yenye vigezo viwili;
• Kuelewa kuwa takwimu ni mchakato wa kufanya uchunguzi na kufanya hitimisho; na • Kuwakilisha utendaji kwa njia mbalimbali.

## Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani:

• Hesabu inaweza kuwa changamoto. Mhimize mtoto wako kutokata tamaa hadi mikakati na zana nyingi ziwe zimekamilika.
• Kumbuka, uzoefu wako na hesabu (iwe chanya au hasi) haufafanui uzoefu wa mtoto wako.
• Njia mojawapo ya kufanikiwa katika hesabu ni kutorudi nyuma. Mhimize mtoto wako kuwa makini, kuuliza maswali na kuendelea kufikia aliye mebele wakati wa darasa.
• Tafuta usaidizi nje ya darasa kutoka kwa mwalimu kabla au baada ya shule na kutoka kwa nyenzo za mtandao.

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

• Iwapo ningetaka kutoa sampuli za wanafunzi katika shule yako ya sekondari miongoni mwa idadi ya watu, ni ipi njia ya haki na uwakilishi ya kufanya hivyo?
• Ikiwa mtaalamu wa hali ya hewa atasema kuna uwezekano wa 90% wa kunyesha kesho, je, hiyo inamaanisha mvua itanyesha kwa hakika?
• Je, ungependa kulipwa senti siku ya kwanza, kisha mara mbili hiyo siku ya pili, kisha mara mbili ya siku ya tatu na kuendelea kwa mwezi mmoja au kupata $10 kwa siku kwa mwezi?

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mwalimu wa Mtoto Wako:

• Je, mtoto wangu ana mapungufu yoyote katika maarifa ya kimsingi ambayo yanasababisha matatizo? Ikiwa ndivyo, ni mapungufu gani hayo na tunawezaje kuziba mapengo hayo?
• Mtoto wangu anapaswa kutumia muda gani kufanya kazi za nyumbani kila usiku?
• Unafikiri ni nini kinachompa mtoto wangu shida zaidi? Je, ninaweza kumsaidiaje kufanya maendeleo katika eneo hili?
• Je, kuna zana zozote (nyenzo, tovuti, video, n.k.) ambazo tunaweza kutumia nyumbani kwa usaidizi wa maudhui?
• Desmos ni nini? Je, kuna vipengele vyovyote ambavyo tunapaswa kutumia mahususi nyumbani kusaidia ujifunzaji darasani?
• Je, ni viwango gani vya ufasaha ambavyo mtoto wangu atakuwa akijifunza mwaka huu? Je, ninawezaje kusaidia ukuaji wa mtoto wangu wa ufasaha katika eneo hilo?

# Kusoma na Kuandika Katika Shule ya Sekondari

## Muhtasari:

Wakati wa shule ya sekondari, wanafunzi watasoma maandishi yanoyozidi kuleta changamoto kutoka kwa tamaduni nyingi, vipindi vya wakati na taaluma na kuandika bidhaa mbalimbali kwa madhumuni na hadhira tofauti. Mtoto wako ata:

- Taja ushahidi unaofaa na wa kina ili kuunga mkono uchanganuzi wa mada;
- Soma kwa karibu ili kuchambua chaguo za maneno ya mwandishi, miundo, maoni na mitazamo ili kutathmini jinsi chaguo hizi zinavyoathiri hadhira;
- Tathmini muundo wa maandishi, tafsiri mbalimbali za vyombo vya habari, mashindano, madai, ushahidi na hoja; na
- Tumia kanuni za Kiingereza sanifu ili kuwa tayari kwa fursa za kuwasiliana katika jamii inayozidi kuongezeka kimataifa.

### Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni::

• Kutoa maelezo kueleza kile maandishi yanasema, na vile vile maana yake;
• Kutazama taarifa katika aina iliyochapishwa na isiyo ya kuchapishwa ili kuongeza ujuzi wa mada;
• Kuelewa jinsi maana ya maneno na misemo yanaweza kuathiri maana ya jumla ya maandishi; na
• Kulinganisha maandishi yaliyoandikwa na waandishi mbalimbali kuhusu mada yanayofanana.

### Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani:

• Mhimize mtoto wako asome na aonyeshe ufahamu wa maandishi mbalimbali ambayo ni ya kawaida kwa maisha ya kila siku, ikijumuisha, lakini sio tu, mapishi, maagizo ya kuunganisha vitu vya nyumbani, taarifa za bili za kila mwezi na taarifa za bima.
• Kuwa na majadiliano kuhusu kile ambacho kila mmoja wenu anasoma au kutazama.
• Mwambie mtoto wako aandike barua, barua pepe na maelezo ya shukrani ambayo yanajumuisha msamiati wa kiwango cha darasa na kuonyesha tahajia sahihi, sarufi na vikao;

### Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

• Ni ujumbe gani au hitimisho gani unaweza kuchukua kutoka kwa maandishi? Je, maneno au miundo anayotumia mwandishi inaathirije ujumbe huo?
• Je, unaweza kushiriki baadhi ya sampuli za bidhaa ulizounda na uniambie kuhusu ulichojifunza?
• Je, vipindi vya habari, matangazo ya biashara, tovuti na makala za magazeti vinatumiaje masimulizi/hadithi kuathiri hadhira?
• Je, unaweza kulinganisha jinsi gani waandishi wawili wanawasiliana kuhusu mada moja?

### Maswali Unayoweza Kumuuliza Mwalimu wa Mtoto Wako:

• Je, mtoto wangu anaelewa vyema usomaji wa ndani na nje ya darasa?
• Je, mtoto wangu ana uwezo gani katika viwango vya kitengo cha sasa?
• Je, kuna fursa zozote za kujitajirisha au usaidizi wa ziada unaopatikana kwa ajili ya mtoto wangu?

# Sayansi Katika Shule ya Sekondari

## Muhtasari:

Wakati wa shule ya sekondari, mtoto wako anapaswa kuendelea kukuza dhana na ujuzi aliojifunza katika madarasa ya kati, kama vile kutumia takwimu kujibu maswali ya kisayansi, kutathmini mapungufu ya modeli na kutumia hesabu kusaidia kutatua matatizo. Mtoto wako ata:

- Pata mafundisho katika sayansi ya kimwili (kemia ya "subatomic" na mnururisho wa sumakuumeme), sayansi ya maisha (mienendo ya mfumo ikolojia, mifumo ya mwili, "DNA") Sayansi ya dunia na anga (jiolojia, falaki, na viumbehai na muundo wa kihandisi (jinsi ya kufafanua matatizo kwa wingi na jinsi ya kutambua mabadiliko wakati wa kutengeneza suluhisho za uhandisi); na
- Kuza ujuzi muhimu wa kutatua matatizo ili kumwandaa mtoto wako kwa ajili ya kufaulu katika aina mbalimbali za masomo ya chuo kikuu na kazi.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni:

• Kutumia jedwali la muda kama chombo cha kueleza na kutabiri sifa za vipengele;
• Kutumia takwimu na dhana za uwezekano katika insha iliyoandikwa inayoeleza jinsi sifa zinavyoonyeshwa katika idadi ya watu;
• Kutumia ushahidi kutoka kwa vimondo kuunda nadharia kuhusu historia ya awali ya Dunia; na
• Kuchanganua changamoto kuu ya kimataifa (upatikanaji wa maji safi) ili kubainisha masuluhisho yanayohusu mahitaji na matakwa ya jamii.

## Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani:

• Muulize mtoto wako kuhusu kile anachojifunza katika darasa la sayansi. Tumia matukio ya sasa kama msingi wa majadiliano.
• Panga safari ya kwenda kwenye jumba la makumbusho la historia ya asili lililo karibu au jumba la sayari.
• Tumia programu za jamii zinazozingatia sayansi ya kimwili, sayansi ya maisha, sayansi ya Dunia na anga na usanifu wa uhandisi.
.

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

• Je, ni matukio gani unayochunguza?
• Je, ni njia zipi ambazo wanadamu wameathiri mazingira?
• Je, unatatua matatizo ya aina gani? Kwa nini wewe/timu/darasa lako ulichagua suluhisho walilofanya?

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mwalimu wa Mtoto Wako:

• Je, ni nyenzo gani ninazoweza kutumia kumsaidia mtoto wangu nyumbani?
• Ni aina gani ya matukio yanayochunguzwa?
• Je, mtoto wangu anapitia aina gani za utafiti wa kisayansi?
• Mtoto wangu anaombwa ajumuisheje ushahidi katika maelezo na hoja?
• Je, kusoma na kuandika na hisabati vinajumuishwaje katika darasa la sayansi?

---

# Masomo ya Kijamii Katika Shule ya Sekondari

## Muhtasari:

Katika shule ya sekondari, wanafunzi wanapewa changamoto ya kujua kusoma na kuandika kiutamaduni na kutayarishwa kwa ushiriki wa kiraia unaowajibika kwa kuwa na ujuzi wa taaluma nne za masomo ya kijamii (uraia, uchumi, jiografia na historia). Mtoto wako ata:

- Elewa maadili na kanuni za kimsingi za jamhuri ya kidemokrasia ya Amerika;
- Elewa athiriano ya wanunuzi na wauzaji katika masoko, utendakazi wa uchumi wa taifa na athiriano ndani ya soko la kimataifa;
- Elewa athari za kitamaduni, kiuchumi, kijamii na kiraia za maisha katika mazingira mengi ya Dunia, na athiriano ya shughuli za binadamu na vipengele vya kimwili kwenye uso wa Dunia; na
- Tumia ujuzi wa kufikiri wa kihistoria ili kukabiliana na matatizo ya leo, kufahamishwa kuhusu kuchukua msimamo thabiti kuhusu masuala na kuleta maana ya ulimwengu uliounganishwa karibu nao.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni:

• Kubainisha uaminifu wa vyanzo vyenye mitazamo tofauti kupitia utafiti wa uchunguzi;
• Kutayarisha na kurekebisha madai na kanusho ili kushughulikia maswali ya maisha halisi na maudhui mahususi;
• Kushiriki katika mijadala ya kiraia ili kushughulikia maswali ya maisha halisi na maudhui mahususi;
• Kukuza hoja, maelezo na mawasiliano ili kushughulikia maswali; na • Kuwasilisha jibu au mpango kazi ili kushughulikia masuala ya maisha halisi, mahususi ya maudhui.

## Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani::

• Mtie moyo mtoto wako aulize maswali. Unapotazama habari, filamu ya hali halisi au kusoma vyombo vya habari vilivyochapishwa na mtoto wako, jadili maswali aliyo nayo na mjadiliane ambapo wanaweza kupata majibu na kujifunza zaidi kuhusu somo.
• Tafuta fursa, kama vile uchaguzi au mijadala ya kisiasa inayoonyeshwa kwenye televisheni, ili kujadili maoni kuhusu masuala ya kisiasa na jinsi maoni hayo yanavyoathiri kufanya maamuzi katika mchakato wa uchaguzi.
• Mhimize mtoto wako kutafiti suala linalokabili jamii yako na awasiliane na mbunge na pendekezo lililo na ujuzi.
• Mfano wa ushiriki wa raia kwa kutafiti wagombeaji kabla ya kupiga kura, kujaza hati za sensa kama familia na kushiriki katika matukio ya ndani.

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

• Ni masuala gani muhimu kwako?
• Ni mazungumzo gani umekuwa nayo darasani ambayo yanakutia moyo, kukuchanganya au kukufanya ushangae?
• Umesoma nini darasani ambacho kilipinga jinsi unavyofikiri?

## Maswali Unayoweza Kumsaidia Mwalimu wa Mtoto Wako:

• Je, unawezaje kuunda na kudumisha mazingira salama ya kujifunzia ambayo yanatoa fursa kwa watoto wote kutoa maoni na mawazo yao?
• Ninawezaje kumwandaa mtoto wangu kushiriki kwa heshima katika mijadala ya darasani ambamo makubaliano yanaweza kufikiwa au yasifikiwe?
• Ni nyenzo gani zinapatikana kwa familia kusaidia kujifunza kuhusu ujuzi wa masomo ya kijamii?